


# GENDER ACTION LEARNING FOR SUSTAINABILITY AT SCALE

Jina la Mwanafunzi

Darasa

Shule au Kikundi

Anuani

Tarehe

GALS @ SCALE

Hivos
people unlimited

## GALS ni nini?


GALS (Mfumo wa Kujifunza Jinsia kwa Vitendo) ni njia ya kijamii ya kujiwezesha, yenye malengo ya kuwapa wanawake pamoja na wanaume kudhibiti zaidi maisha yao kama mtu binafsi, kaya, jamii na maendeleo ya shirika.

Watu huendeleza maono yao wenyewe na barabara kwaajili ya mabadiliko. Watu huongeza usawa wa kijinsia kwenye kaya zao ili kila mtu awe na furaha zaidi na afikie uwezo wake wa juu kabisa. Wanashirikishana njia hii ili kuwasaidia wale wanaowapenda na pia kuwasaidia wengine kufikia maono yao na jamii yenye usawa na yenye upekee.



## Nyenzo ya 1: Ndoto yangu

## Nyenzo ya 2: Barabara ya mafanikio



**Hatua 1 Ndoto**
Ndoto yangu ni nini? (chora ndani ya duara juu upande wa kulia)

**Hatua 2 Mahali sasa**
Mahali nilipo sasa ni wapi? (chora ndani ya duara chini upande wa kushoto).
Unganisha maduara mawili kwa kutumia mistari miwili kwa ajili ya barabara.

**Hatua 3 Fursa na changamoto**
Fursa zangu ni zipi? (10+ weka juu)
Changamoto zangu ni zipi? (weka chini)

**Hatua 4 Lengo la muda**
Lengo la muda maalum ni nini? (mfano mwaka, miezi 3 nk) Malengo ya muda mfupi ni nini (mfano miezi 3/6/9 au miezi 1/2/3 nk)

**Hatua 5 Shuguli**
Shughuli gani utakazofanya? (chora katikati ya malengo ya muda mfupi)

**Hatua 6 Matunda**
Fuatilia mafanikio kwa matunda ya rangi nyekundu. Fikiria namna ya kuboresha.

## Nyenzo ya 3 MTI WA USAWA WA JINSIA

**Hatua 1 Shina:**

Nani yuko kwenye kaya yako? (Chora katikati ya mistari miwili katikati ya karatasi.)

**Hatua 2 Mizizi: Shughuli**

Shughuli gani mwanamke wanafanya? Za kuleta kipato? (Mzizi wa mwisho upande wa kushoto) Za nyumbani? (Mzizi wa pili kutoka kushoto)

Shughuli gani mwanaume wanafanya? Za kuleta kipato? (Mzizi wa mwisho upande wa kulia) Za nyumbani? (Mzizi wa pili kutoka kulia)

Shughuli gani tunafanya pamoja? (Mzizi wa katikati)

**Hatua 3 Matawi: Matumizi**

Matumizi gani mwanamke wanafanya? Binafsi? (Tawi la mwisho upande wa kushoto) Kwa ajili ya nyumbani? (Tawi la pili kutoka kushoto)

Matumizi gani mwanaume wanafanya? Binafsi? (Tawi wa mwisho upande wa kulia) Kwa ajili ya nyumbani? (Tawi la pili kutoka kulia)

Matumizi gani tunafanya pamoja kwa ajili ya nyumbani? (Mzizi wa katikati)

**Hatua 4 Nguvu kwenye shina: mali na maamuzi**

Mali gani zinamilikiwa na mwanamke? na mwanaume? pamoja?

Maamuzi gani yanafanyika na mwanmwake? na mwanaume? pamoja?


(Chora vitu vya mwanamke upande wa kushoto wa shina, vya mwanaume upande wa kulia, vya pamoja katikati ya shina)


Chora upande wa kushoto wa shina)

**Hatua 5 Matunda**

Tufanye mabadliko gani kwenye shughuli, matumizi, umiliki wa mali na maamuzi ili mti uwe sawa kwa mwanamke na mwanaume? Zungushia duara kwa rangi ya kijani kuonyesha matunda mabichi.

**Hatua 6 Mabadliko yakitokea zungushia matunda ya kijani kwa rangi nyekundu kama matunda yaliyoiva.**





## Nyenzo ya 4 RAMANI YA UWEZESHAJI WA UONGOZI

**Hatua 1 Mimi ni nani/nikoje? katikati ya duara.**

Nijichore katikati ya duara.

**Hatua 2 Watu au taasisi gani muhimu zinazonisaidia au kunirudisha nyuma?**

Wakina nani watanisaidia na kunizuia mimi? (Wachore watu hao na taasisi kwenye maduara kuzunguka duara la katikati. Wale wa muhimu wanakuwa karibu na duara langu/la kati.)

**Hatua 3 Mahusiano gani yaliyopo kati yangu na watu au taaasisi hizo? Mishale**

Je ni upendo? (mshale mwekundu) Ni pesa? (mshale wa kijani) Nguvu? (mshale mweusi) Kuelekea upande gani? (weka ncha ya mshale) Je ni kubwa au ndogo? (chora mshale mnene wa mwembamba nuktanukta)

**Hatua 4 Kuna mbadiliko**

Mabadiliko gani? Je mahusiano gani nina furaha nayo? (Weka alama yenye sura ya kufurahi). Mahusiano gani ninataka kuyabadilisha? (Weka alama yenye sura ya kusikitika.)

**Hatua 5 Nani nitamshirikisha njia hii? Matunda ya kijani**

Watu gani naweza kuwasaidia? Watu gani naweza kuwabadilisha? Zungushia au weka namba kwa watu hao au taasisi.

**Hatua 6** Mtandao wangu wa uongozi ni mkubwa kiasi gani? Fuatilia watu wapi niliowashirikisha. (Zungushia haya kwa rangi nyekundu.) Je na wao wamewa shirikisha wengine? Kufuatilia matunda mekundu. (Weka duara jekundu liwe pana sana.) Weka namba kama vile utando wa buibui.

## Mkataba wa Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Binadamu za Wanawake.

Haki 1: Uhuru wa kutokua na vurugu


Haki 2: Usawa katika kufanya maamuzi

Haki 3: Haki sawa za umiliki wa mali

Haki 4: Uhuru wa mawazo, kutoka sehemu moja mpaka nyingine na kuungana

Haki 5: Usawa wa kazi na burudani

*Imesainiwa na Serikali ya Tanzania 1998*






**Mawasiliano ya ndani ya jamii**

**Grace Murungi**
**Moshi (0787 298 641)**
**Charles Kainkwa**
**Arusha (0754 058 694)**

**Mtandao**

**wa GALS@scale kwaajili ya filamu na rasilimali**

**www.galsatscale.net**



